VIGEZO NA MASHARTI YA M-TIBA KUSHIRIKI MPANGO WA KUWEZESHA WAMAMA WAJAWAZITO KULIPIA GHARAMA ZA HUDUMA ZA AFYA YA MAMA NA MTOTO KWA KUTUMIA SIMU YA MKONONI

Karibu kushiriki kwenye Mpango wa kumuwezesha mama mjamzito kulipia gharama za huduma za afya ya mama na mtoto kiliniki (RCH TOP UP). Lengo mahususi la mpango huu ni kumuwezesha mama mjamzito kupata kwa haraka na urahisi huduma za afya ya mama na mtoto aendapo kiliniki na kuzilipia kupitia akaunti yake maalum kwenye simu yake ya mkononi. Ili kushiriki vema huna budi kutumia M-TIBA. Mama anahakikishiwa kupata huduma stahiki kipindi chote cha ujauzito mpaka atakapojifungua mtoto na hali kadhalika kuendelea kupata huduma za afya baadaa ya kujifungua. Aidha, kupitia mpango huu utasaidia juhudi za kuokoa afya na uhai wa mama na mtoto pia hivyo kupunguza vifo vya wamama wajawazito na watoto. Ili uweze kushiriki kwenye mpango huu huna budi kuwa tayari kutumia akaunti ya fao la unufaikaji wa wa kulipia gharama za matibabu kupitia akaunti yako maalum kwenye simu yako ya mkononi. Katika Mpango utawezesha kufuatilia kwa karibu kwa kutumia teknolojia ya simu ya mkononi kubaini na kuhakiki huduma mama mjamzito unazozipata kipindi cha ujauzito wako na baada ya kujifungua. Utakaposajiliwa katika mpango huu itatafsiriwa umesoma, umeelewa na kukubaliana na masharti na vigezo vya kushiriki kwenye mpango huu kwa hiari yako mwenyewe.

1. MAANA NA TAFSIRI YA BAADHI YA MANENO

1.2 “Akaunti ya kidigitali ya Afya ya Mama na Mtoto (RCH TOP UP)” ni akaunti dhahania inayotolewa kutoka kwenye mfumo wa kidigitali wa M-TIBA unaomilikiwa na CarePay kumuwezesha mama kutumia mafao ya kwenye akaunti ya simu ya mkononi kulipia baadhi ya huduma za afya ya mama na mtoto aendapo kiliniki.

1.3 “PHARMACCESS”: Ni shiriki lisilo la kiserikali lenye makao makuu yake nchini Uholanzi lenye lengo mahususi kusaidia wakazi wanaoishi chini ya jangwa ya Sahara barani Afrika kupata huduma bora za afya na kwa gharama nafuu.

1.4 “CAREPAY”: ni kampuni yenye mfumo wa kidigitali unaowaunganisha wagonjwa, watoa huduma za afya na wafadhili katika kufanya kazi kwa pamoja kuwezesha kutoa huduma bora za afya na malipo kwa kutumia akaunti ya maalumu ya simu ya mkononi.

1.5 Wewe ni mama mjamzito aliyekuabali masharti na vigezo na ameandikishwa kwa ajili ya kunufaika na kutumia “Akaunti ya Afya ya Mama na Mtoto” kwenye Mpango huu (RCH TOP UP).

1.6 Vituo vya kutolea Huduma za Afya: ni watoa huduma za afya ya mama na mtoto kwako wewe kipindi cha ujauzito na baadda ya kujifungua mtoto. Aidha utaweza kupata huduma hizo katika moja ya kiliniki zilizopo katika Hospitali ya wilaya ya St. Joseph au Kibosho Hospitali.

1.7 “Wabia katika Mpango huu ni PharmAccess, CarePay, watoa huduma za afya na wewe mama mjamzito ambao wanashirikiana kutekeleza kwa pamoja

2. MPANGO WA MAMA MJAMZITO KULIPIA HUDUMA ZA AFYA KUTUMIA AKAUNTI MAALUM YA SIMU YA MKONONI.

2.1 (RCH TOP UP) Ni Mpango unaokuwezesha wewe mama Mjamzito kupata na kulipia baadhi ya huduma zilizoainishwa za kiliniki ya afya ya mama na mtoto kwa kutumia akaunti maalumu ya simu ya mkononi. Aidha, fedha hizo zitawekwa kwenye akaunti yako na mfadhili na utazitumia tu kwenye Kliniki uliyosajiliwa kupata huduma

- Mpango huu (RCH TOP UP) unakuwezesha kulipia na hivyo kunufaika na huduma zifuatazo katika Kliniki iliyopo kwenye hospitali uliyoichagua;
- Mahudhurio yote manne ya msingi ya kipindi cha ujauzito
- Huduma zote na vipimo vyote awali vikiwemo vinavyotakiwa kulipia maabara
- Kipimo cha Ultra Sound (Kitafanyika mara moja TU)
- Virutubisho vya madini Chuma kipindi cha ujauzito
- Matibabu ya magonjwa yatokanayo na ujauzito: Presha, Upungufu wa Damu, maambukizi kwa njia ya mkojo.
- Matibabu kwa matatizo yatakayoabainika kipindi cha kuhudhuria huduma za kiliniki na Kujifungua Treatment of complications in Antenatal care and during delivery
- Kumuona mtoa huduma mara 2 kuapata huduma ya mama na mtoto baada ya kujifungua
- Chanjo kwa mtoto/watoto wachanga mpaka week ya 14.

2.2 Utakaposajiliwa katika Mpango huu (RCH TOP UP), kumbuka utanufaika kwa kipindi cha mwaka mmoja tu kupata huduma za mama na mtoto.

3 ELIGIBILITY

3.1 Lazima uwe na ujauzito usiozidi miezi sita
3.2 Muhimu kuishi karibu na makazi ya hospitali utakayohudhuria huduma za Kiliniki
3.3 Lazima uhudhurie mahudhurio yako yote ya kiliniki katika hospitali uliyoichagua
3.4 Lazima uwe umesajiliwa tayari kwenye (RCH TOP UP) ili usajiliwe na kunufaika na mpango
3.5 Lazima uwe tayari kutumia simu ya mkononi kulipia huduma za afya kila uendapo kiliniki

4 USAJILI

4.1 Kusajiliwa utapewa maelezo ya kina na wakala wa Mpango wa Usajili wa wamama wajawazito watakaolipia huduma za afya katika kiliniki kwa kutumia simu ya mkononi. Mawakala hawa wameajiriwa na PharmAccess.
4.2 Maelekezo jinsi ya kupata huduma kwa wateja kutoka (RCH TOP UP), tafadhali piga simu namba **0800754002.**

5 JINSI YA KUPATA HUDUMA

5.1 Akaunti yako ya (RCH TOP UP) itatumika tu katika hospitali uliyosajiliwa kama ilivyoanishwa katika kipingele namba 1.8 cha masharti na vigezo hivi.
5.2 Wewe kama mnufaikaji utaweza kupata wasaha wa kumuongeza mtoto wako uliyemzaa kama mtegemezi ili kunufaika na mafao ya Mpango Huu wa RCH TOP UP.
5.3 Ni muhimu kukumbuka kuwa gharama yoyote itakayozidi itakayotokana na kupewa/kutaka huduma nje ya zinazolipiwa na Mpango huu (RCH TOP UP) itabidi ZILIPWE NA WEWE.

6 USALAMA NA USIRI WA TAARIFA ZAKO

6.1 Unaposhiriki na kutumia hudma za RCH TOP UP kupitia akaunti ya Mpango wa kidigitali wa Afya ya Mama na Mtoto kupata huduma za afya katika kiliniki, inatasfiriwa umewaamini CarePay wanaweza kutunza taarifa zako za matibabu yako yote kipindi unachoshiriki na baada kushiriki katika Mpango huu. PharmAccess na CarePay wanakuhakikishia usalama na usiri wa taarifa zako zitakazokuwa

zikichukuliwa kupitia mfumo wetu wa kidigitali. Taarifa zako utakazotoa zitaweza kutumiwa na wabia wengine wanaohusika na Mpango huu(RCH TOP UP) wakiwemo watoa huduma za afya katika Hospitali unayohudhuria kiliniki na mfadhili.

Taarfia za usajili

6.2 Kuwezesha usajili unahitajika kufungua akaunti ya (RCH TOP UP) amabapo utahitajika kutoa jina lako, tarehe ya kuzaliwa,jinsi, namba simu ya mkononi kama unayo,kitambulisho na nenosiri. Hii itsaidia CarePay kua na taarifa zako zote sahihi katika kufanikisha usajili na majukumu yaliyomo kwenye mkataba huu.

Matumizi ya taarifa zako

6.3 Kwa kutumia RCH TOP UP ni muhimu kufahamu kua CarePay wanakusanya taarifa zako na huzitumia kukusajili na kukuwezesha kupata huduma zitokanazo na RCH TOP UP. Hivyo taarifa hizi huwezesha kusimamia na kuangalia akaunti yako, huduma na mawasiliano kwa wateja, upatikanaji wa huduma, kuwezesha taarifa za malipo ya watoa huduma katika vituo vya afya

6.4 Taarifa unazitoa au zipatikanapo kipindi cha kupata huduma za afya husimamiwa, kudhibitiwa na hushirikishwa kwa wabia wa mradi huu wakiwemo watoa huduma za afya.

6.5 Taarifa zako binafsi zinazokusanywa; wanaoweza kuzipata na kuziona ni kiliniki ya hospitali uliyoichagua na wabia wanaotekeleza mpango huu. Na taarifa hizi zitatumika kwa ajili ya shughuli za mpango huu na si vingenevyo.

Meseji za CarePay

6.6 Kwa kutumia RCH TOP UP utakuwa unatumiwa taarifa au matangazo mbalimbali pia tafiti kutoka CarePay kwa njia ya SMS au kupigiwa simu. Aidha una haki ya kujitoa pindi unapohitaji kufanya hivyo. Piga *150*30# nenda “matengenezo” au piga huduma kwa wateja namba 0800754002

Kushirikishwa taarifa zako kwa wadau wasio wa Mpango huu

6.7 CarePay haitatoa taarifa zako zozote kwa wasio wadau wa moja kwa moja wa Mpango huu bila ruhusa yako ila TU kama ilivyoelezewa na kuelekezwa katika masharti na vigezo katika mkataba huu kisheria kwa ajili ya shughuli za kiundeshaji za RCH TOP UP chini ya CarePay. CarePay itabakia kuwajibika kutunza taarifa zako wakati wote.

6.8 CarePay inaweza kushirikisha taarifa za mtegemezi wako katika masuala yatokanayo na gharama ya matibabu na huduma za afya zilizopatiwa kwake /kwao, madai na malipo yaliyofanyika, gharama za makato zilizofanyika. CarePay haitatoa taarifa za zozote za kitabibu ikiwemo historia yake ya matibabu ambayo imeshawahi kufanyika LABDA iwe imeombwa na mtegemezi wako mwenyewe.

Muda wa Kuhifadhi Taarifa zako

6.9 CAREPAY wanaweza kuweka/kuhifadhi taarifa zako kwa muda usiozidi miaka saba kama inavyotakiwa kisheria. Una haki na unaweza kupata taarifa zako zitokanazo na mpango huu pindi utakapozihitaji kwa kupiha simu namba 0800754002

Utafiti

6.10 CarePay inabakia kwa na haki kisheria kutumia taarifa zinazopatikana katika mpango huu na repoti zake kushirikisha wadau wake wa maendeleo bila ya kutumia majina ya washiriki (wagonjwa/wanufaika wa programu hii). Taaifa hizi pia zatatumika katika shughuli za kiuendeshaji za CarePay ikiwa na lengo la kufanya tahimini ili kuboresha ubora na upatikanaji wa huduma za afya chini ya programu mbalimbali zilizo chini ya RCH TOP UP.

Mengineyo katika masula ya taarifa

6.11 CarePay inabakia kwa na haki kisheria kutumia taarifa zinazopatikana katika mpango huu na kuzitoa hadharani bila ya kutaja majina ya washiriki (wagonjwa/wanufaika wa programu hii) ikiwamo wadau wake ikiwemo serikali ya Jamuhuri ya Kenya. Hii itaweza kutaarifiwa kuwa moja ya program zainaozendeshwa chini ya RCH TOP UP hivyo taarifa juu huduma za afya zilizolipiwa na kutolewa ili kuboresha huduma, pia kwa masuala ya kitakwimu na kitafiti.

6.12 CarePay imeasili njia madhubuti za kitaalamu na kisheria za kudhibiti na kulinda taarifa zako binafsi hivyo kutoweza kudukuliwa wala kutumiwa na watu /taasisi zisizo husika.

Haki zako

6.13 Una haki ya kujitoa katika Mpango huu wakati wowote kwa kuwasiliana na huduma kwa wateja wa RCH TOP UP kwa kupiga namba 0800754002.

6.14 Pia kama ukipenda kuhakiki taarifa zako au wategemezi wako tafadhali wasiliana na huduma kwa wateja ya M-TIBA namba 0800754002.

7 TAHADHARI

7.1 Ingawa PharmAccess na wabia wa Mpango huu(RCH TOP UP) watafanya jitihada za kulinda taarifa zako zote kitaalamu na kwa uangalifu wa hali ya juu bado inapenda kutoa angalizo kua kushiriki katika mpango na utoaji wa taarifa zako ni kwa usalama wako mwenyewe. PharmAccess au CarerPay haitahusika na upotevu au uharibu wa taarifa zozote utakaohusishwa kutokana kutumia akaunti yako ya kidigitali ya afya ya mama nma mtoto aidha kupitia virusi, tojans, n.k PharmAccess haitahusika na wizi wowote wa kifisadi kupitia mtandao wa simu ya mkononi /namna nyinginyeo itakayopelekea kuibiwa fedha zako katika akaunti yako ya kifedha ya simu ya mkononi.

7.2 Unawajibika katika kufanya marekebisho ya taarifa zako katika RCH TO UP

7.3 Kwa kupata huduma za afya kupitia mpango huu (RCH TOP UP) unatafsiriwa kua umekubali kujiunga na mpango huu bila ya kushurutishwa na hivyo huna haki kisheria kuishitaki PharmAccess au CarePay katika hilo.

7.4 Kwa kushiriki kwako unakubali kua hospitali na waajiri wake wote hawatahusika na upotevu au uharibifu utokanao na;

7.4.1 Tukio lolote liloshirikisha nguvu nje ya uwezo au uelewa wa watoa huduma hospitalini yakiwemo ugaidi, uadui, mashitaka ya viwanda

7.4.2 Uharibifu wowote ule au upotevu wa taarifa zako kwenye simu yako utokanao na programu haribifu, virusi,Trojans, kutoka katika vifaa vya kidigitali kwenda kwenye simu yako unayoitumia kwa program ya RCH TOP UP .

7.4.3 Upotevu wowote ule utakaotokana na kutopata taarifa sahihi au kupata huduma kuliko nje ya uwezo wa CarePay kusaidia.

7.4.4 Upotetevu wowote kutoka katika mifumo ya teknohama nje ya CarePay

7.5 CarePay haitausika na vitendo vyovyote vya kifissadi au wizi wa kimitandao utakaotohusisha upotevu wa fedha zako katika akaunti yako ya kifedha ya simu ya mkononi.

7.6 CarePay haitahusika na vitendo visivyo vya kiungwana vitakavyofanywa na watoa huduma wanaoshiriki Mpango huu wakati wa kupata huduma.

8 HAKI YA KUJITOA KATIKA MKATABA HUU

8.1 Aidha Wewe (Mnufaika), PharmAccess na CarePay mna haki ya kusitisha utoaji wa huduma za afya kupitia mpango huu wa kutumia akaunti ya kidigitali wa Afya ya Mama na Mtoto wakati wowote. Hili linaweza kufanikishwa kama ifuatavyo-

8.2 Tafadhali piga namba ya simu 0800754002 ili kutolewa au kujitoa mwenyewe kwa kupiga *150*30#. Chagua RCH TOP UP kisha TOKA

8.3 Ikiwa umejitoa katika mpango huu, mafao yaliyo kwenye akauti yako yatarudishwa CarePay hivyo hautaweza kupata huduma za afya ya mama na mtoto bure kama ilivyokua awali.

9 MIGOGORO NA UTATUZI KISHERIA

9.1 Kama utata au mgogoro wowote unaohusiana na mpango huu unaweza kuwasiliana na dawati la huduma kwa wateja la RCH TOP UP kwa kupiga simu namba 0800754002

9.2 Migogoro yoyote itakayojitokeza katika Mpango au itokanayo na masharti na vigezo ainishwa katika mkataba itajadiliwa na pande zote mbili kama invyotakiwa.

9.3 Uamuzi utakaoafikiwa na baraza la usuluhishi huo ndio utakua usuluhishi wa mwisho kwa pande zote mbili.

9.4 Vigezo na masharti haya yote yataongozwa chini ya sheria za nchi ya Tanzania

10 MABADILIKO YA MASHARTI NA VIGEZO VYA MPANGO HUU

10.1 Hata hivyo, katika vigezo na masharti tajwa, CarePay anabakia kua na haki ya kutunza, kuondoa au kuondoa upatikanaji wa bidhaa, maudhui au vitu vingine vihusivyo Mpango wa kulipia huduma za afya ya mama na mtoto kwa kutumia simu ya mkononi muda wowote ule bila ya kutoa taarifa. Pia CarePay wanaweza kusitisha au kupunguza baadhi ya upatikanaji wa huduma zilizomo katika mpango huu bila taarifa yoyote kwako au kuwajibishwa.

11 AKAUNTI NA TAARIFA ZAKE YOUR ACCOUNT AND ACCOUNT INFORMATION

11.1 Tafadhali usitoe taarifda za akaunti yako kwa mtu mwingine. Unawajibika kutunza taarifa zako zote ikiwemo usalama wake. Vitendo vyovyote vitakavyojitokeza dhidi ya akaunti yako tafadhali watarifu CarePay mapema. Aidha PharmAccess hawatawajibika kwa upotevu wowote utokanao nan a kudukuliwa/kuchukuliwa/kutumiwa taarifa zako kwenye akaunti yako bila ya ruhusa yako.

11.2 Isipokuwa imesemwa vinginevyo, la sivyo taarifa, promosheni, bonas na mafao mengineyo yapo katika programu husika. Taarifa zitokanazo na kutumia menyu ya USSD au mobile application hazina mashiko au athari kisheria na zinatoa tu muhtasari wa masharti na vigezo vya program husika.

12 MENGINEYO

12.1 Masharti na vigezo vilivyobainishwa katika mkataba huu ni mapya na hakuna uhusiano na mikataba mingeneyo ambayo ulishawahi kuingia na CarePay.

12.2 Aidha unaweza kuathririka na masharti na vigezo yakayongezeka kutokana na huduma za mshiriki mwenza katika Mpango huu

12.3 Ikiwa sehemu ya vigezo na masharti yatakua batili au kutoweza kutekelezeka, kipengele husika kitajadiliwa na kuakisiwa kisheria bila kupoteza/kuathiria ualisia na maana yake iliyokusudiwa hapo awali.